REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Wednesday, 15th September, 2021

The House met at the Assembly Chambers at 10.24 a.m.

[The Speaker (Hon. Patrick Waigwa) in the Chair]

PRAYERS

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

CHANGE OF HOUSE LEADERSHIP

Speaker: Hon. Members, I wish to bring to your attention a communication that I have received from the Jubilee Party, Majority Chief Whip, Hon. Charumbo Kaparo, and I will read it. This is on Jubilee Party leadership at the County Assembly. The Jubilee Party National Management Committee, made the following resolution on the leadership of Laikipia County Assembly, after wide consultations and in accordance with the Laikipia County Assembly Standing Order 19.

The Leader of Majority Hon. Peter Thomi Waigwa, and Deputy Majority Leader, Hon. John Mutahi Muritu, shall retain their respective positions in leadership. That is the written by Hon. Raphael Tuju, EGH, Secretary General, and is well copied to the Clerk of the County Assembly and as well to the Governor of Laikipia County. It is my belief that the Chief Whip has been able to communicate the same in your caucus.

Hon. Stephen Nderitu: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Kwanza nashukuru kwa sababu ya hio taarifa imefanyika. Nafikiria hio taarifa ni sheria na kwa hivyo mimi nilikuwa nafikiria kwa sababu umetoa hio taarifa na chama imesema hivyo, nikiangalia hii kiti mbele yangu iko wazi.

Wale ambao wametajwa wako katika Bunge hili, mimi ningeomba kama hii kiti ingekaliwa ndiyo Bunge ionekane iko sawasawa na ionekane viti zote zimekaliwa ndiyo tuweze kuendelea na jambo lingine. Ningetaka utoe amri kama huyo Kiongozi wa Wengi hayuko, Naibu Kiongozi wa Wengi yuko ndani ya hili Bunge, akalie hiki kiti ndiyo tuendelee.

Speaker: It is not me to make a show of dust, I think the people use the power that they have been given.

Hon. Simon Kanyutu: Mr. Speaker, I thank you for the communication because I was shocked yesterday to learn through the twitter from the Jubilee Party. Now I was wondering, we are getting it from the twitter and the Speaker has not mentioned it here. I congratulate you for making the reading, I was waiting if it could not have been communicated we would have raised that concern. Am very happy for you and we are ready to work together to ensure we move forward for the remaining eleven months.

Hon. Mutahi Muritu: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Nakushukuru wewe kwa nafasi hio na nikushukuru pia kwa kuwa umeongozwa na busara. Cheo ni dhamana, na pili tangu huu mgororo uanze kwenye hii Bunge, nilikuomba sana lakini nashukuru chama changu cha Jubilee kwa kuchukua uamuzi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kama kuna kitu chochote kinahitajika kufanyika, na nimshukuru kiranja wangu katika Bunge, ni mzee mwenye busara. Hilo jambo limekuwa ni ngumu sana hata yeye kwa kutamka kwa sababu unaelewa kile kitu kinaendelea. Niwaombe Wabunge, kama kuna kosa limefanyika mimi nimekosea mtu na nimeomba sana, mimi naomba mtu yeyote anisamehe.

Tunapofanya kitu chochote kinachohusiana na sheria, ni kitu cha maana sana tunapofuata utaratibu. Umekuwa ukitushauri hapa kwamba hii ni nyumba ya heshima, kwa hivyo mimi ninachokiomba sisi Bunge, muda wetu umeisha na kwa sababu umeisha, kwa nini kila saa tunakuwa na malumbano kuchao?.

Mheshimiwa Spika, hii chama yetu na ukiangalia mustakabali wa nchi yetu, sasa hivi kitu kinachohitajika zaidi ni kuwapa wananchi wetu huduma na wala si mapambano. Mapambano haisaidii na kwa hivyo mimi nashukuru chama changu na kiongozi wangu Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Kiranja wangu, na pia wewe kama hio ndiyo maamuzi ndiyo ilitolewa na chombo cha hali ya juu sana katika taifa hili naishukuru sana.

Mimi niwaombe Wajumbe, wacheni baadaye mimi naongea kwa niaba ya Kiongozi wa Wengi. Nimewasiliana na yeye baada ya kikao tutaweza kufanya mawasiliano kuwaita Wajumbe wote tukae pamoja, kama nimekukwaza tusameheane ili tuweze kusonga mbele. Tukiendelea kulumbana hapa na wananchi wetu wanatuangalia tumekuwa tukikaa kwa nidhamu sana na mimi nihakikishie kila mtu ambaye amekuwa kwenye Bunge hili, sisi kama viongozi hatuna nia mbaya na mtu yeyote.

Tutendewe haki lakini baadaye pamoja na kiranja wa Bunge, mawasiliano yatafanywa Wajumbe wote wakae pamoja. Kama nimekukwaza unisamehe, na pia kama umenikwaza tusameheane ili tuweze kupeleka Laikipia Mbele. Tofauti na hapo na hii Bunge tutakuwa kicheko mpaka kwenye Mtaa.

Kwa hayo mengi ama machache, Kiongozi wa Wengi atakuweko na yuko karibu, mimi niko tayari kuwafanyia kazi. Nimekuwa nikilalamika nilisulubiwa msalabani bila hata kuelezwa chochote lakini mwenyezi mungu, *subarahan wataala* ameweza kunifanyia haki na kuweza kunitoa aibu ambayo nilitwikwa.

Hon. Christopher Mark: Thank you, Hon. Speaker. Just to congratulate those who have been put in leadership, and there is always one thing i would like to remember. As Members of this Assembly in terms of leadership we serve at the pleasure of the party, so congratulations to the new leadership, you have a big task ahead to unite this House. We have eleven months to go and they should be nothing else but development-oriented, oversight of the Executive, legislation and many bills so that at least the 2017-2022 Assembly can be one that has a mark. Thank you.

Speaker: Hon. Salma Hussein then Hon. Wakahiu.

Hon. Salma Zamzam: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipa nafasi pia nitilie mchango wangu kwa uteuzi mpya wa Kiongozi wa Walio Wengi na Naibu wake katika Bunge la Kaunti ya Laikipia. Tunashukuru kwa vile leo umetoa maamuzi, jinsi ambavyo ndugu yangu Kagondu amesema na kusoma ripoti. Tuliona jana kwenye mitandao tukafikiri ni propaganda, bali tunamrudishia aliyetoa hayo maamuzi, Raphael Tuju. Jinsi ambavyo ndugu yangu Mheshimiwa Chris aliweza kusikia mashinani kulivyo na akaamua kutoa maamuzi kama kiranja wa chama.

Bwana Spika, vile ambavyo wenzangu wameweza kuongea, hapo mbeleni tulikuwa na msukosuko na ninaomba walioteuliwa kuongoza hili Bunge tuwe na usawa na haki kwa sababu hakuna aliye kijikiongozi na aliye kiongozi katika hili Bunge. Leo hii, Mheshimiwa Thomi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

akichukua usukani na Mheshimiwa Mutahi Muritu, ukweli usemwe, sisi tulioachwa nje tulikandamizwa na tunaomba mchukue usukani na kuweka kila mtu kwenye usawa na haki kuanzia kesho.

Hakuna tunayetaka afinyiliwe wala aonekane sio mtu kwa vile ametolewa. Yeye pia ni Mheshimiwa na alitumwa hapa na watu wake kuwakilisha wengine. Lazima heshima iwekwe. Hata waliowekwa na kutolewa madarakani na chama lazima tuwape heshima kwa sababu wao pia ni viongozi wa hii Kaunti. Sina mengi ila kumrudishia Mungu shukrani, na kurudisha shukrani kwa Chama cha Jubilee kinachoongozwa na Uhuru Muigai Kenyatta.

Kama mteule wa wachache katika Bunge la Kaunti ya Laikipia, siwezi kupingana na kiongozi wangu wa chama, Uhuru Muigai Kenyatta ama kitu ambacho kimetoka kwenye ofisi. Siwezi kupinga na siogopi kusema wala kuongea kule kando, nasimama mia kwa mia na Uhuru Muigai Kenyatta. Vile ambavyo chama kitafanya, tulikubali wazuri walipowekwa bali sasa imeonekana haifai na wengine waendelee na safari. Wacha tuwape kongole na tuendelee kama Bunge moja na tuliowekwa nje tupate nafasi.

Hon. Wilson Wakahiu: Asante Bwana Spika. Sitaki kunena mengi ila tu kuwapongeza waliorudishiwa viti vyao na chama. Niseme hivi, isiwe kwamba wakati mtu anaona kama amefinyiliwa kidogo inakuwa kama sherehe kwa wengine na wengine wetu kukaa kama tunawashusha. Ninakumbuka sisi wenyewe katika hili Bunge tumepitia safari ndefu sana. Tumefika mahali, kwa kutofautiana kwetu, kunakuwa kama vita. Hicho ni kitu ambacho si kizuri. Huenda leo ni mimi na kesho ni wewe.

Ningeomba, kama ambavyo Mheshimiwa Zamzam amesema, waliorudishwa kwenye viti sio kusema watakuwa wakubwa wa wale wengine. Walioachishwa vyeo sio kwamba wafinyike. Kama alivyosema, mimi nilikuwa mwenyekiti kwenye kamati fulani ya Bunge na nilipotolewa, ilikuwa sherehe kwa wengine. Hilo si jambo nzuri kwenye hili Bunge. Kama Mheshimiwa ametolewa kutoka kwenye cheo cha Kiongozi wa Walio Wengi hebu naye apate nafasi nyingine awe sawa na sisi. Hilo tu ndilo litasaidia hili Bunge. Hii shida yote imeletwa na sherehe na mambo mengine ya vyombo vya habari tuliyofanya baadaye. Hakuna mshindi wala aliyeshindwa. Sisi sote tuketi chini; sio lazima Mheshimiwa Wakahiu apewe kiti cha Mwenyekiti wa Bajeti ama gani, bali ningependa pia nijisikie kama Mheshimiwa Lochimidi ama Mheshimiwa Kagondu. Hio ndio itafanya hili Bunge kuendelea kwa njia inayofaa katika miezi tuliyobakisha. Tutakuja kufurahia tutakapokuwa tunawachana hapa, ahsante.

Speaker: Hon. Lochimidi, Hon. Irene John, Hon. Mugweru and Hon. Robert Maina.

Hon. Lochimidi Essokon: Bwana Spika, ninaanza kwa shukrani zangu kwa chama kwa kumteua tena Kiongozi wa Walio Wengi pamoja na mdogo wake. Ningeomba Wajumbe wenzangu huu uwe mwamko mpya, tuweke tofauti zetu za kisiasa kando na kufanyia watu wetu kazi. Tuwache kulumbana kwa vile tuna wakati mfupi.

Waliopata nafasi, tuwaheshimu waliokuwa hapo mbeleni. Tofauti zetu za kulumbana hapa na pale ziishe kabisa. Nasema tu asante kwa kiongozi wa chama chetu ambaye ni Uhuru Muigai Kenyatta pamoja na Raphael Tuju kwa nafasi waliyochukua. Kwa hivyo tuweke tofauti zetu kando na tushikane tena kuendelea mbele ili watu wetu waweze kufanyiwa kazi. Ahsante sana, naunga mkono.

Speaker: Hon. Wachuka, then Hon. Mugweru then Hon. Maina

Hon. Irene Wachuka: Asante sana, Bwana Spika. kwanza nashukuru kwa hii nafasi ambayo umenipa. Namshukuru pia katibu mkuu wetu, Bwana Raphael Tuju ambaye aliketi na kufikiria mambo ya Bunge la Kaunti ya Laikipia. Namshukuru pia Rais wa Jamhuri ya Kenya,

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Uhuru Muigai Kenyatta aliyenifanya niwe hapa kwenye hili Bunge, nashukuru chama cha Jubilee ambacho kimenifanya niwe hapa leo. Nataka tu kuongea mambo mawili au matatu kama kigogo wa siasa.

Asiyekubali kushindwa, sio mshindani. Kuingia kwenye hili Bunge sio kusema eti kuna vita hapa. Kiongozi wa Walio Wengi ambaye alikuwa Kiongozi wa Walio Wengi mbeleni, Mheshimiwa Peter Thomi Waigwa pamoja na Mheshimiwa John Mutahi Muritu ambao wamerudishwa kwenye viti; Bwana Joseph Kiguru aliyetoka Igwamiti na mdogo wake ambaye ni Veronica Muthoni Ikunyua, waketi chini na kukubali kwa sababu ni chama kimetoa uamuzi. Hicho ni kitu ambacho kila mtu aliona jana kwenye runinga tukadhani ni yale mambo watu huandika tu lakini mwishowe tukaona ni chama kimetoa uamuzi.

Bwana Spika, nakupongeza kwa sababu wewe huongei maneno tu bali unangoja mambo yaje. Cha kusema tu kwa vile Kiongozi wa Walio Wengi hayuko hapa, kupitia kiti chako, singetaka Naibu wa Kiongozi wa Walio Wengi atoke kabla sijasema hayo maneno kwa sababu nilikuwa nataka asikize kwa niaba ya Kiongozi wa Walio Wengi. Kwa nini wamerudi kwenye viti? Kama ambavyo Mheshimiwa Wakahiu amesema, tukae kama Nyumba moja. Kama ulipata kiti, mimi sikupata kiti chochote lakini nimeketi tu kwenye hili Bunge nikikumbuka kuwa nililetwa hapa na chama nifanyie *Wanjiku* kazi.

Usione kwa vile wewe hukupata kiti na umerudi tena kunakuwa na mgogoro. Ningetaka wakae chini na kufikiria huu ni mwamko mpya. Kusema wamerudi si kusema tuanze vita. Ningetaka tufanye kazi pamoja, tushikane na Gavana tufanye kazi pamoja. Juzi, kupitia Kiti chako, Bwana Spika, mimi nilikuwa napinga mkopo hadi dakika ya mwisho. Sio kusema mimi ni adui wa Gavana, huo ni msimamo wangu. Sio kusema eti sitafanya kazi na wale wengine. Hayo mambo yaliisha na sasa tuko pamoja, tufanye kazi pamoja.

Nawauliza Wajumbe wenzangu, hii mikutano ya usiku inayofanywa hapa iishe, watu waendelee na kazi. Wachuka usiwaite watu watatu au wanne na kufanya mikutano kumsema sijui Spika ama yule mwingine, tafadhali Waheshimiwa hayo yameisha na *Wanjiku* angali anatuangalia.

Hon. Simon Kanyutu: Bwana Spika ningependa kuelezwa, haya mambo ya mikutano ya usiku, kama Mheshimiwa Irene anaweza kueleza vizuri ili ijulikane, mikutano ya usiku ni gani?

Hon. Irene Wachuka: Mheshimiwa Spika, mimi naongea ninachokijua. Nimejitaja, hata Wachuka niache mikutano yangu, sikutaja mtu. Nasema hata mimi naweza kuwa naitana kwenye mikutano hata hapa kwenye Bunge, naitana hapa nje au naingia kwenye chumba cha mikutano au kile chumba cha juu cha mikutano au kuita mkutano hapa nje. Hicho si kitu ninachoweza kujibu.

Tunataka kumaliza hii mikutano, tuwe kitu kimoja. Hata mimi Hon. Wachuka, nisiite mikutano huku nje, kama ni mikutano tunahitaji iwe ni moja. Tungetaka wakati kiongozi wa wengi atakapokuja, tukae chini sisi wote kwa mkutano mmoja, tusameheane. Kama nilikukosea kama vile Hon. Mutahi alivyosema, unisamehe na pia mimi nikusamehe, Ila si kusimama hapa kutaja watu. Na kama wewe unajua unafanya mikutano, kutoka leo uwache hiyo mikutano ya usiku, tuwe kitu kimoja. Asante Bwana Spika.

[The Speaker (Hon. Patrick Waigwa) left the Chair]

[The Temporary Speaker (Hon. Chris Mark) took the Chair]

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Temporary Speaker (Chris Mark): Ni sawa tuwache mikutano ya usiku, lakini ya maombi tusiache. Maombi tunaweza omba, kwa sababu maombi ya usiku iko na nguvu sana.

Hon. Daniel Mugweru: Thank you, Hon. Speaker. Before I make my contribution, I feared when I heard you say meetings are bad, whereas I know I might even hold this meeting today, or every other day we will be having meetings. It only depends which kind of meetings you are having. You may be having family meetings at night, prayer meetings and all that. It is allowed anytime and anyday, as long as you observe the rules in the country.

I also wish to take this opportunity, one, to thank the party for what has been done and the communication that you have made Mr. Speaker. It is upon us Honourable Members, as a House, to stand up and work together to see that Laikipia goes at least a mile ahead. Leadership or any position that one gets in this House, is a responsibility given to you on behalf of all of us. Any position that one gets in this House, should always be used in a good way and serve the Members of this House Mr. Speaker.

Mr. Speaker, whenever you get a position, it comes with a lot of tasks. It is upon the leadership of the House, and upon the Majority and as well as the Deputy Majority Leader, to stand up beyond division. That is the best leadership one can give to any institution, House, and any other place. The first thing is to stand up beyond and above the division that is there or being mentioned, that way you are able to lead the people in the best way Mr. Speaker.

I congratulate the two Honourable Members, and it is still our prayer that they will stand above the division or any test that is moving around this House. Today we may be singing a song with the Majority, or the Deputy Majority Leader, or anyone else, but now they have a position, it is their responsibility to rise above everything else and use that task to serve everybody. We as Honourable Members, must understand today that even if you are cordial with so and so, once they are given a position to serve everyone, things may be different and you might blame that person for no reasons.

In the elections that happened in 2017 where I was elected, we had several teams in Umande ward, but now when I got the position I had to serve everyone. The ones who were opposing me, those that were supporting me and the ones that were neutral. I had to go beyond everybody and every group to enable me serve everyone appropriately Mr. speaker.

For anyone to serve people or to stand as a leader, you must go beyond some of the things that you have been doing. Even the statements that you make as a leader, you might find yourself not doing the same. Today when you get a responsibility to lead this House, as a Majority Leader, you are told you are the leader of the government business in the House. Whether you feel like you want to oppose, sometimes you will be forced to swallow your decisions, because the role dictates what you are supposed to do Mr. Speaker.

All leaders must have time to listen to everybody and to accommodate everyone's opinion so that they may lead this House in the best way. We do not want wrangles anymore, we are only having like 3 months and after that, everyone in this House will go to the ground. In one way or the other you will find the House, has no quorum as expected. The leadership must stand to accommodate everyone's idea, because we need this House, to stand to the end.

If we start wrangles today, by the time we are in the month of April, we will be having problems in this House because everyone will be going there. From August some of us may not be elected, and others will be re-elected. This is the biggest task the leadership has been given to unite us in a way such that even after the elections if I lose we will relate well and live in harmony, thereafter.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker this is the high time to know that the kind of task they have been given, is not just the leadership of the House, for this remaining 8 or 9 months. They need to show us direction and start something that will re unite us as Members today and forever. It will be unfortunate when I hear that somebody probably from the furthest part of Laikipia, needs me most and I cannot be available just because we did not have proper leadership.

It is our high time to stand beyond division and as well the expectation, we show a different kind of leadership from what people expected, exceeding the expectations. That is what we require in this House and I believe the leadership of the House will do something. As the Deputy Majority Leader has said on behalf of the Majority leader, we are going to have a meeting for all Members, that will be the best for this House and will help us move ahead. I congratulate them, hoping that they will go even beyond the expectations and as well they will go above this House, so that we may have a good name. Thank you.

Hon. Robert Maina Asante, Mheshimiwa Spika. Kwa kunipa nafasi hii na langu kwanza ni kukushukuru wewe kwa kufanya taarifa ambayo ilitoka katika chama chetu cha Jubilee, kupitia Katibu wetu Mheshimiwa Raphael Tuju. Nataka pia kupongeza wale ambao wamerudishwa kwa viti vyao. Wajue ya kwamba ili ifike hicho kiwango cha kutolewa, labda kulionekana kuna shida kidogo na labda sheria haikutumika kulingana na chama chetu cha Jubilee.

Bwana Spika, nilikuwa tu katika hili Bunge, wakati mwingine nikisema *" what goes around, comes around"* kwa hivyo niambie Mheshimiwa mwenzangu Hon. Mutahi, ajue ya kwamba wakati wako kwenye hizi viti, wakuwe na usawa wa kufanya mambo inayvopaswa. Kutoshanisha watu sio kama vile tuliona katika uongozi huo mwingine wa kukejeli watu. Kucheka wengine huku nje, mfahamu ya kwamba Waheshimiwa wote wako sawa, hakuna yule yuko juu wala chini ya mwingine.

Mfahamu ya kwamba tumebakisha miezi kumi, na hatutakuwa hapa wakati wote. Wengi wetu tutakimbia kule mashinani Mheshimiwa Spika. Ningetaka kuwambia wajumbe hawa, tunapokuwa kule mashinani tuheshimu wengine wale tumechaguliwa na wao na tuheshimu wale tuko hili Bunge.

Mheshimiwa Spika, naweza kuangalia ni kana kwamba hauwezi au hauwezi fika kiwango fulani kwa ofisi fulani kule juu, lakini hivi karibuni sitasema ni nani niliyesaidia. Alinipata kwa ofisi fulani na hakuwa anajua ya kwamba ninaweza kuwa na uwezo hata nikitoka Ngobit na nikaweza kumsaidia. Kwa hivyo tuheshimiane kama Wajumbe na tujue ya kwamba tumebakisha miezi kumi ili twende kule mashinani. Wale ambao watabahatika wapate viti na wale ambao hawatapata bahati waende wakalime, lakini tutaishi kuwa ndugu na dada.

Tutaishi kuwa tunasaidiana na kwa hivyo niweze kuwapongeza hao ambao wamerudishiwa viti, na wafanye kazi kwa bidii kwa sababu tumebakisha miezi kumi. Hii safari tuiendeshe kwa haraka ili tuweze kufanyia Wanalaikipia kazi. Asante.

Hon. Chalumbo Kaparo: Asante, sana Mheshimiwa Spika. La kwanza nataka nishukuru Mwenyezi Mungu kabla niseme mambo ingine yoyote. La pili nakushukuru Bwana Spika kwa ile hatua ambayo umechukua leo na pia vile unaendesha kazi ya hili Bunge la Laikipia sawa sawa. Kabla nipongeze wale ambao Mwenyezi Mungu amechagua, Kiongozi wa Walio Wengi na naibu wake, sina aibu kwa sababu kuna haki ya kusema hivyo.

Ninashukuru pia kwa sababu wakati ambapo nilipata barua kama kiranja wa Bunge na Jubilee pia leo asubuhi, niliileta mbio kwa Bwana Spika nikifuata sheria. Hakuna haja kumangamanga huko. Wakati mimi nilikuwa natafuta kiti mwaka wa 2017, nilikuwa napiga

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

makofi huko kwa Jubilee nikiomba kiti na hicho ndicho kimenisababisha kuwa hapa siku ya leo. Bado nashukuru, naamini na ninapenda Jubilee kwa sababu wakiamua leo watachukua cheti changu, basi nitaosha mkono pale na kusema ya kwamba nimenyolewa na Jubilee.

Bwana Spika, Nimefurahi kusikia Mheshimiwa mmoja akisema ya kwamba wengine wakiona wengine wamenyolewa watakuwa na furaha na kicheko ambacho hawakuwa nacho kila siku. Tujaribu tuwache hiyo kwa sababu leo ni mimi na kesho haijulikani ni nani. Kwa hivyo yale ya muhimu, wale ambao wamerudishiwa viti vyao na Jubilee, tusimame na kutii sheria ya Jubilee ilivyo.

Leo mimi ninaomba Wabunge wetu tutafute nafasi tuketi pamoja na tuzungumze kwa lugha moja kama watu wa Laikipia. Mimi niliona kwa runinga huko Olmoran wengine wakifa na wengine wanachomewa manyumba, wengine wanalala kwa makanisa, na wengine wanatembea usiku na mchana wakibeba bunduki. Badala tuongee maneno ya hiyo shida, jana niliona watu wakiandamana kwa Mheshimiwa Suge huko Rumuruti wakichoma pikipiki za wengine na kuongea maneno ambayo sio mazuri.

Ni vizuri ieleweke ya kwamba kama wewe unalima mahindi, hiyo ndiyo ng'ombe yako. Kama wewe unachunga ng'ombe, hiyo ndiyo shamba lako. Ni lazima kila mtu aheshimu mali ya mtu mwingine kwa sababu hakuna haja mimi kama Kaparo nipeleke ng'ombe zangu kwa mwenye anayelima mahindi. Hiyo sio haki na sio maendeleo. Kila mtu ajue ya kwamba jirani yuko. Juzi niliona Laikipia ikiwa kwa hiyo orodha ambayo lilikuwa ikionyeshana zile kaunti ambazo kiangazi imekuwa mbaya. Siku ya Kwanza Laikipia ilikuwa lakini na siku ya pili nikatafuta Laikipia na sikuipata na sisi tuko na njaa. Mwenye anang'oa hayo mambo kutoka Laikipia anafaa aje Laikipia apate ng'ombe zikifaa.

Kwa hivyo Waheshimiwa siku ya leo ni siku kuu ambapo tunafaa kama Waheshimiwa tutafute siku na tuingie kwa Bunge letu tutafute suluhisho na kupeleka kaunti yetu mbele wala sio maneno ya kusema ni nani mkubwa kuliko mwingine au ni nani mnono kuliko mwingine au ni nani ameisha nywele kichwa kuliko mwingine. Hakuna haja ya hayo. Tunafaa kuendeleza Laikipia mbele na ikiwezekana tuache porojo mingi. Hakuna mtu hapa ambaye anasimama mahali na kusema anajua kuliko wengine. Wewe unajua nyumba yako na mwingine anajua kwake.

Sijui ni nini kilichoingia Kaunti ya Laikipia lakini tunafaa kuomba Mungu. Hakuna haja nijifiche kwa kioo lakini ninaonekana. Tuendeshe kaunti sawa sawa na tuombe Mungu. Siku hizi nikiangalia luninga kitu cha kwanza ni Laikipia hadi ninashindwa ni shetani yupi ambaye imeingia Laikipia. Narudia kusema ya kwamba yeyote ambaye amefinywa kwa kiti chochote, unajua kama wewe umefinywa na haujasema, utaendelea kufinywa sawa sawa mpaka useme ili uonekane ni wapi ulipofinywa. Kwa hivyo tuendeshe maneno sawa sawa. Watu ni kuongea na wale ambao wamefinywa waongee ili wanaorekebisha maneno warekebishe ili hii dunia ikae sawa sawa.

Nashukuru kwa sababu sitaki porojo kama wakati ule mwingine. Ninasema ya kwamba sitaki kukanyaga Jubilee tena na kesi zingine. Mimi nimemalizana na huko na ndio maana nilipopata barua leo nilipeleka bila kuiweka kwa mfuko wangu. Hiyo ndiyo sauti yangu na kauli ambayo nimefanya leo. Jubilee imeniamurisha nipatiane hiyo barua kwa Spika na kama hangetangaza leo ningesimama na kusema ya kwamba Spika yuko na barua kwa mfuko. Uzuri ametangaza na kwa hivyo tunafaa kuendelea na kazi.

Nimemalizia hapo na ni vizuri tuweke Bunge letu sawa sawa kwa kuongea kwa sauti moja. Karibu niseme ya kwamba siku hizi Mheshimiwa Spika hana barakoa. Naangalia barakoa yake na kuona ni kama ndevu. Namalizia kwa kusema, kwa sababu haya yameisha

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kwa amani, tunafaa kutafuta siku hata kama ni leo ama kesho tukae pamoja kwa sababu sisi ni jamii moja na Waheshimiwa katika hili Bunge la Laikipia. Asante.

Hon. Catherine Nyokabi: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipatia hii nafasi. Kwanza nishukuru Maulana kwa kuwa hii siku tuko wazima zote. Nimesimama hapa niunge uamuzi wa chama ambacho kilichonileta katika hili Bunge ambacho ni chama cha Jubilee na kinaongoza na Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta. Ninapongeza Kiongozi wa Walio Wengi na naibu wake Mheshimiwa John Muritu na niseme ya kwamba tuko pamoja na tutafanya kazi.

Tungeomba kwa sababu Mungu amewarudishia viti tuweze kuungana pamoja. Wacheni tukae kama dada na ndugu wa hili Bunge kwa sababu hasira ni hasara. Wakati ambao umebaki ni mchache sana na hakuna haja ya kushinda tukigombana kila wakati. Tufanye kazi pamoja ili tuweze kuendeleza Laikipia mbele. Kwa hayo machache naunga mkono na niwapongeze tena. Asante.

Hon. George Meshami: Asante sana, Bwana Spika. Nami pia nasimama na ningependa kuambia Mungu ni asante kwa ile kazi jema ambayo amefanya kulingana na ule wakati ambapo Bunge letu la Laikipia limekuwa likipigana. Mimi sikuwa napata raha kwa sababu kwa hiyo miaka yote minne tulikuwa tunapendana kama dada na ndugu na tumekuwa tukifanya kazi pamoja na pia kujuliana hali, ukiwa umekosa Bunge ungepata Waheshimiwa kama sita wakikupigia simu wakiuliza uko wapi.

Tulikuwa na upendo kwa hiyo miaka minne lakini shetani ilipokuja kutuvuruga, kila mmoja aliyekuwa rafiki wako wa karibu wakaanza kuwa maadui. Hii siku ya leo mimi nashukuru Mungu sana kwa sababu ametenda. Sisi Wamaasai husema ya kwamba kichwa cha nyumba ni mwanaume. Kwa hivyo namaanisha ya kwamba hiyo vurugu ndio tunaona katika Laikipia yetu kwa sababu hata sisi viongozi wateule tumeanza kupigana. Ndio sababu shetani ikatupitia katikati.

Bwana Spika, leo mimi nataka uunganishe hili Bunge pamoja na viongozi ambao wamerudishiwa viti wakiwemo Kiongozi wa Walio Wengi na naibu wake. Kitu cha kwanza muende mketi chini na muombane msamaha kwa sababu labda mmoja wenu amekosea mwingine na ndio sababu Bunge lilivurugika kwa sababu mlipata kutofautiana. Viongozi wake chini waombane msamaha na kisha mkimaliza mteremke kwetu na mtupatanishe. Mimi nikikumbuka tangu shida ianze hadi siku ya leo hatujawahi kukaa kwa chumba cha mikutano. Hicho chumba cha mikutano huwa kama ni kama hakuna watu ambao hukaa huko. Wakati ninapotoka hapa naenda tu kukunywa chai. Naomba viongozi wakutane pamoja tusameheane na tupate kuendesha wanalaikipia ambao waliotuchagua kwa njia nzuri. Kwa hayo machache, Mungu wa Mbinguni awabariki.

Hon. Joseph Suge: Asante, Mheshimiwa Spika kwa hii nafasi ili niweze kuchangia kuhusiana na barua ambayo ilitumwa katika hili Bunge na kinara wa chama cha Jubilee. Kwanza kabisa ningependa kuwapongeza waliorejeshewa viti vyao wakiwemo ni Kiongozi wa walio Wengi pamoja na naibu wake.

Mheshimiwa Spika, Waswahili husema ya kwamba “yaliyopita sio ndwele, tugange yajayo”. Sisi kama viongozi wa hili Bunge tunalo jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu tumekuwa mahali hapa kwa miaka minne na kwa miaka miwili iliyopita, hili Bunge liliweza kukaa kwa pamoja bila vurugu na tukachaguana. Ilipofika mwaka wa tatu, hapo ndipo shida iliweza kuanza. La muhimu ni tujue ya kwamba baada ya malumbano huwa pia na nafasi ya maridhiano. Wengi wamesema ya kwamba mmoja alikwaruza mwingine na kuna nafasi ya kusameheana ili safari iweze kutimia vizuri.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Tofauti ya Bunge isiwe ni tofauti ambayo inaweza kufika mahali pa kusema tubadilishe na kufanya A, B, C, D. Mimi ni kiongozi na nimekuwa katika hili Bunge kwa serikali la kwanza na pia nikawezeshwa na Mwenyezi Mungu kuwa katika Bunge la pili. Niliona mambo ambayo pengine ni tofauti kidogo lakini la muhimu ni ya kwamba viongozi wanafaa kuwa kitu kimoja na kuongea kitu kimoja.

Mheshimiwa Kaparo ametaja kuhusu shida ambazo zimekumba Kaunti yetu. Sisi kama viongozi tunafaa kuwa katika mstari wa mbele tunapoenda kuongea na wananchi na kuwaleta pamoja. Sio vyema kama vile mmoja amesema ya kwamba unaweza kujificha kwa kioo. Watu wakienda mashinani wasipokuwa kitu kimoja, mazao hayawi mazuri. Huu ni ukurasa mpya na ninaambia hawa viongozi wawe kitu kimoja ili hili Bunge liweze kuwa kitu kimoja ili hii miezi kumi na moja ambayo imezalia iwe ni wakati wa manufaa kwa wakaaji wa Laikipia na nafasi nzuri yetu kujipanga kwa sababu ya mambo ya siasa.

Tungependa kwa Bunge hilo lingine ambalo litakuja, kama Mungu atatuwezesha tuweze kuwa mahali hapa, hatuwezi kuwa mahali hapa kama tunalaumiana bila kutaka kusaidia wenzetu. Katika uongozi kila mmoja ana nafasi ya kusaidia mwingine na kwa hayo machache ninaunga mkono na niseme ya kwamba ni wakati mzuri wa watu kusemezana. Mimi nikiwa mzee, mambo yangu huwa machache. Nimekuwa nikisema tangu mwanzo ya kwamba kabla ya kuchukua hatua bila kuangalia na kuzingatia, ni vizuri watu kushauriana na hicho ni kitu ambacho nimekuwa nikiongelelea kwa muda mrefu. Mara nyingi huwa naambiwa ya kwamba ninakosea na huwa nakubali lakini maridhiano na umoja ni kitu cha maana. Nashukuru.

BILL

THE LAIKIPIA COUNTY CLIMATE CHANGE BILL, 2021

Second Reading

Hon. Simon Kanyutu: Thank you, Mr. Speaker. I beg to move;

THAT the Laikipia County Climate Change Bill, 2021(Laikipia County Bills No. 6) be now read for a second time.

Mr. Speaker, this is a bill that will assist our county. The object of this Act is to create a mechanism to improve, sustain financial climate change activities, programs and projects in the county through;

(a) Creating a fund in the county for the purpose of facilitating establishment of a mechanism to finance climate change activities, programs and projects in the county.

(b) Mainstreaming climate change in different sectors.

(c) Coordinating collection and dissemination of climate change information to the public to create awareness and preparedness.

(d) Initiating and coordinating financing of climate change adaptation and mitigation activities at the community level in the county.

(e) Enhancing climate finance mechanism in the county.

(f) Facilitating community- initiated climate change adaptation and mitigation activities in the county.

(g) Facilitating planning for climate change adaptation and mitigation in the county planning and budgetary framework.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(h) Seeking and receiving grants from national and international entities, the National Government, the County Government and other relevant organisations.

(i) Providing for procedural and administrative matters.

(j) Providing support from the National Climate Change Policy and Legislative framework and

(k) Coordinating collection and dissemination of climate change information to the public to create awareness and preparedness.

Mr. Speaker, I call upon the Hon. Member for Salama to second.

Hon. Wilson Wakahiu: Thank you, Mr. Speaker. I second this bill as moved by the Chair for Agriculture, Water and Natural Resources which I am a Member of the committee. Mr. Speaker, we have gone through this document for sometimes and we have engaged various stakeholders concerning the same.

Mr. Speaker, I believe the County Assembly will approve this document so that we have one of the best bills in this county. Mr. Speaker, as you are aware, since 2017 I doubt whether we have more than five bills in this House. I support the issue of the Hon. Chair concerning the same because we are doing our best to make sure that this bill have been brought in this House.

I request Hon. Members to support and adopt to make sure that we have moved to the next level. Thank you, I second.

(Question proposed)

Hon. George Meshami: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Nasimama kuunga mkono kusoma kwa mara ya pili ya hii sheria. Hii ni sheria ambayo itasaidia Laikipia tukipitisha. Tukipitisha hii sheria tutakuwa na usaidizi wa fedha kutoka kwa shirika na Serikali Kuu. Kulingana na hii sheria Bunge la Kaunti ya Laikipia itakuwa ikipitisha pesa ya kusaidia mabadiliko ya hali ya anga katika Kaunti ya Laikipia. Naunga mkono kusomwa kwa mara ya pili. Asante.

Hon. Salma Zamzam: Asante sana, Mheshimiwa Spika kwa kunipea nafasi ili nichangie sheria ya mabadiliko ya hali ya anga ambayo inasomwa kwa mara ya pili katika Bunge la Laikipia. Hii sheria imekuja kwa wakati ambao unafaa. Tumeona kulikuwa na janga la kuvamiwa kwa nzige na Korona ambayo inaharibu hali ya fedha. Kwa sasa Laikipia nzima iko na kiangazi. Juzi tu ndio tuliweza kupata mvua na ni vizuri kuwe na sheria ya kusaidia wafugaji na wakulima katika Kaunti ya Laikipia ili tusiwe na mzozo ambao tunaona katika Kaunti ya Laikipia.

Tukiwa na sheria kama hii, itatuongoza wakati Waheshimiwa wanaleta ripoti ya kupigana na kiangazi. Huo mjadala utaweza kuangaliwa kwa sababu kutakuwa na pesa ambayo tutakuwa tumetenga. Pia kutakuwa na pesa kutoka kwa Serikali Kuu ili kupambana na mabadiliko ya hali ya anga katika Kaunti ya Laikipia. Tukirudishia Kamati ni wakati wa kutekeleza hii sheria.

Tunapomalizia hatua za hii sheria, ni vyema Gavana Ndiritu Muriithi kutia sahihi kwa haraka kwa sababu tumeona tulikuwa na sheria ya janga na hadi sasa hivi haijawekwa sahihi na ingesaidia pakubwa katika Kaunti ya Laikipia haswa saa hii tuko na vita Ol Moran. Ni vizuri aweze kutia sahihi ili iweze kutumika. Hata tukiangalia Kaskazini, Mashariki na Magharibi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mwa Laikipia watu wanakufa njaa, wanyama pia wanakufa na hii sheria ingetusaidia pakubwa kwa kupatia watu nyasi na kupatia watu liche.

Hata chakula ingepelekwa kwa shule tungekuwa na hii sheria. Asante sana, Mheshimiwa Spika. Naunga mkono na naomba wajumbe wenzangu waweze kuunga mkono iweze kupita ili iweze kutumika katika Kaunti ya Laikipia. Asante.

Hon. Joseph Suge: Thank you, Mr. Speaker. I also stand in support of the second reading of this bill in this Assembly. This bill is of great importance to the people of this great county of Laikipia. I have seen the purpose of this bill is one to Coordinating collection and dissemination of climate change information to the public to create awareness and preparedness. This is one of the great functions of this Act because we have seen the challenges the Laikipians are facing.

We have seen conflicts within the corners of this county that arise due to the prolonged droughts. This bill will create a chance for the county to interact, equip our people and enlighten them on how they can be prepared to tackle some of these challenges. Mr. Speaker, in the National Government, we had the Arid and Semi-Arid Ministry which was dealing with the issues of climate change.

We have had the support of the Climate Smart Agriculture which is trying to coordinate and support our farmers. For now they can also mitigate these challenges. Having the bill in place, I know Laikipians will benefit more from these programmes. I support the bill, thank you.

Temporary Speaker (Hon. Chris Mark): I now call upon the mover to make the response.

Hon. Simon Kanyutu: Thank you, Mr. Speaker. I congratulate all the Hon. Members who have contributed on the same. This is a bill that will be beneficial to our county and it will assist us. It will also facilitate the issues that are hurting us at the moment. I call upon all the Hon. Members to approve the second reading so that in the evening we can probably come for the Committee of the Whole and make the amendments that are required. Thank you.

(Question put and agreed to)

(The bill was read a second time and committed to a Committee of the Whole)

ADJOURNMENT

Temporary Speaker (Hon. Chris Mark): The sitting of this House stands adjourned until today afternoon Wednesday, 15th September, 2021 at 2.30 p.m.

The House rose at 11.25 a.m

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*